Swahili

## Je, ulijua?

# Kaswende ni maambukizo makubwa ambayo yanaweza kukudhuru wewe na mtoto wako.

Ikiwa wewe ni mja mzito au unapanga kuzaa mtoto, kupima mapema ni muhimu sana ili kuhakikisha huambukizi kaswende kwa mtoto wako.



**Kaswende** ni maambukizo ya zinaa (STI) ambayo yanaambukizwa kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine wakati wa kujamiana. Wanawake wengi zaidi wenye umri wa miaka 15 hadi 44 wanaipata. Jua jinsi unavyoweza kujikinga wewe na wapendwa wako.

### Huenda usiwe na dalili zozote

Watu wengine wanaweza wasijisikie kuwa wanaumwa au hawajui kuwa wana kaswende.

Angalia kama una vidonda au donda, upele, maumivu ya misuli na ya viungo, maumivu ya kichwa na uchovu.

### Pata kipimo mara kwa mara

Vipimo vya kaswende ni vipimo muhimu vya kawaida wakati wa ujauzito. Tembelea daktari yako, mkunga au mtoaji wako wa huduma ya akina mama ili uweze kupimwa.

Hakuna aibu katika kupimwa – ni ya faragha, haraka na rahisi.

### Matibabu

Matibabu ni rahisi – dawa huondoa maambukizo na ni salama kwako na kwa mtoto wako.

Bila matibabu, kaswende inaweza kuathiri afya yako na afya ya mtoto wako. Hii ni pamoja na uwezekano wa kifo cha mtoto wako.

### Kaa salama

Fanya ngono salama – tumia kondomu na mpenzi mpya na upimwe mara kwa mara.

Wapenzi pia wanapaswa kupimwa mara kwa mara ili kuzuia kaswende kurudi kwako au kuwaambukiza wengine.

Ikiwa hujisikii vizuri kuwasiliana na wapenzi wako wewe mwenyewe, unaweza kutembelea kwa **www.letthemknow.org.au** ili kupata ushauri au kuzungumza na daktari yako.

**Changanua msimbo wa QR ili kujua zaidi kuhusu kaswende na afya ya wanawake.**

MULTICULTURAL HIV & HEPATITIS SERVICE

**Wilaya ya Afya ya Mahali ya Sydney ya Kusini Magharibi**

Huduma ya Kukuza Afya

NSW GOVERNMENT